**Learning by Ear – Jobs and Education**

**Elimu ya Chuo kikuu- Hadithi ya Malaika/ Episode 05**

**Mwandishi: Njoki C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri:Eric Ponda**

| Wahusika: | |
|---|---|
| Msimulizi | - Mwanamume |
| Malaika | - Msichana miaka-19 |
| Mhadhiri | - Miaka 48 hivi |
| Daniel | - Mwanafunzi miaka 20 |
| Cindy | - Mkaazi mwenza wa Malaika- Miaka 19 |
| Mshauri wa wanafunzi | - Mhadhiri miaka 50 |
| Mwanafunzi | - Miaka- 20- katika darasa la Malaika. |

**INTRO**

**MUZIKI WA UTANGULIZI**

**MSIMULIZI** Hujambo na karibu tena katika makala ya tano ya mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear kuhusu kazi na mafunzo. Katika kipindi kilichotangulia Malaika amerejea nyumbani kwa likizo na kukukuta wajibu na majukumu yake yanaendelea kubadilika na kuanza kutekeleza yale anayojifunza chuoni nyumbani kwao. Wakati huo huo anatembelea

shule alikosomea na kuwahimiza wanafunzi wenzake kusoma kwa bidii na kuanzisha mradi wa kutoa mafunzo ya Komputa kwa wanafunzi hao. Kwa ujasiri Malaika pia anaepuka jaribio jingine la wazazi wake la kutaka kumuoza mapema. Sasa amerejea chuoni, lakini je, ni vipi atakabiliana na masomo chuoni?

**SCENE 1: OFISINI MWA MHADHIRI ANAYETOA USHAURI KWA WANAFUNZI:**

**SFX: ANABISHA MLANGONI**

MHADHIRI: (***kutoka ndani***) Ingia!

**SFX: Mlango unafunguliwa**

MHADHIRI: Ndio, msichana nikusaidieje ?

MALAIKA Samahani nilitaka kukuuliza kuhusu ule mpango wa mafunzo ya utendaji nyanjani kwa wanafunzi na wewe kama mshauri wa wanafunzi nadhani unaweza kunisaidia.

MHADHIRI Bila shaka. Huo ni mpango wa lazima. Ni moja wapo ya masharti kwa kila mwanafunzi anayekamilisha masomo kwamba aende kwa

mafunzo haya ya utendaji nyanjani. Wengine pia wamefanya, kwa hiyo sioni tatizo gani kwako wewe.

MALAIKA — Labda hunielewi ninakotoka. Mimi nina tatizo kubwa. Sijui mtu yeyote mjini licha ya shirika.

MHADHIRI — Mpango huu ni lazima hapa chuoni, kwa hivyo ni bora uanze kutafuta mashirika hayo. Ofisi yangu itakupa msaada unaohitaji, lakini ni jukumu lako kutafuta mashirika hayo wewe mwenyewe. Hapa chuoni huwa tunawafunza jinsi ya kujitegemea mbali na elimu ya kawaida. Tunataka mwende huko nje kufanya utafiti na kutuletea. Sisi huwa tunawasaidia kuwaandikia barua za kuwajulisha kwa wakuu wa mashirika mbali mbali, lakini ni lazima mwanafunzi afanye bidii ya kutafuta kampuni hizi yeye mwenyewe. Sio eti tunawatupa la!

**MUZIKI**

**MSIMULIZI** — Malaika sasa ametambua kwamba hawezi kuepuka mpango huu wa mafunzo ya utendaji nyanjani. Bado amechanganyikiwa na hajui afanye nini. Anatafuta ushauri kutoka kwa rafiki yake Daniel.

## SCENE TWO: CHUONI

**SFX: Sauti za ndege wakiimba, watu na magari barabarani vikisikika kwa mbali.**

DANIEL — Malaika.. si vigumu hivyo! Unaweza kuanza kutafuta katika kitabu cha orodha ya majina na anuani au hata katika mtandao wa intaneti…..

MALAIKA — Oh, Daniel, Inanitatiza!

DANIEL — Malaika, ehh, itazidi kukuchanganya iwapo utaendelea kulichukulia suala hili kuwa gumu..

MALAIKA — Sasa tuanzie wapi?

DANIEL — Tatizo lako wewe ni kwamba unataka kurudi nyuma kila wakati ….. hapa,….angalia hapa..!

**SOUND: WAKICHAKURA MAKARATASI**

DANIEL — Hii ni orodha niliyoitayarisha ya majina na anuani za mashirika na kampuni ambako wanafunzi wenzangu walikwenda kufanya mpango huu mwaka uliopita.

MALAIKA — Oooh… Daniel, wewe ni malaika… rafiki mkubwa wa kutegemewa.

**SOUND: SAUTI YA BUSU**

MALAIKA — Ningelifanyaje bila ya wewe?

DANIEL — Naamini umenibusu sasa hivi hapa kwenye shavu….?

MALAIKA — Nimekubusu kweli?

DANIEL — Ndio umenibusu, hapa hapa, hapa kwenye shavu? Sasa pia ni lazima nami nikubusu.

MALAIKA — (***wakitekerenyana na kuchezacheza***) Hapana huwezi…….

DANIEL — ***(akicheka)*** ….. Kwa nini, lazima nikubusu….

MALAIKA AND DANIEL — (***wakiendelea kutekerenyana na kufukuzana***)

**MUZIKI**

**MSIMULIZI** — Kwa mara nyingine Daniel amekuwa msaada mkubwa sana kwa Malaika. Na sasa urafiki wao umeanza kukita mizizi. Changamoto zinazomkabili Malaika pia zinawakabili wanafunzi wengine na zimekuwepo tangu mwanzoni. Njia pekee ya kukabiliana na changamoto hizi ni kujifunza kutoka kwa wenzake.

**SCENE 3: KATIKA VYUMBA VYA MAKAAZI: CHUMBANI KWA CINDY NA MALAIKA:**

CINDY (***akiwa na usingizi***) Malaika, kumekuwa usiku nenda ukalale.

MALAIKA Ni lazima nijiandae kwa mtihani... Lakini Cindy si hata wewe una mtihani wiki hii?

CINDY Ndio.

MALAIKA Kisha?

CINDY Ahh, tayari nimepita!

MALAIKA Unamaanisha nini? Hebu nikwambie mwenzangu, iwapo hutaacha uvivu wako na kutoka kitandani kuja kusoma, utaanguka mtihani na mimi sitakuwepo utakapokuwa ukilia machozi.

CINDY Nani mimi? Nianguke mtihani? Nimekwambia tayari nimepita. Na hilo nakuhakikishia...

MALAIKA Hebu nizungumzie kwa lugha inayoeleweka Cindy!

CINDY Angalia hapa… hebu angalia .

**SFX: Akichukua funguo. Na kufungua kabati. Makaratasi yachakurwa.**

MALAIKA — ***(akipigwa na butwaa)*** Oh, Mungu wangu!… Haya ni majibu ya mtihani… umeyapata wapi?

CINDY — Wewe msichana nadhani hujachanuka. Changamka…! Kuna njia nyingi tu za kupita mtihani …

MALAIKA — Hapana hapana Cindy sitaki kusikia haya! Hebu chukua makaratasi yako. Huo ni udanganyifu…! Mimi nataka nipite mtihani kutokana na juhudi zangu za kusoma na kuelimika. Sio udanganyifu. Ni makosa sana!

CINDY — ***(akiwa ameudhika)*** Sawa mimi si Malaika kama wewe. Lakini sijali mradi nimepata shahada yangu ya digrii, sina haja na mambo mengine. Kwa hivyo usiku mwema na usome kwa bidii.

**MSIMULIZI** — Maadili ya Malaika sasa yameanza kukabiliwa na mtihani mkubwa. Je aendelee kushikilia maadili haya, au kufuata njia ya Cindy. Maisha yamemgeukia. Hata hivyo ni kutokana na msimamo wake utakaoweza kumuongoza katika maisha yake chuoni.

**MUZIKI**

| | |
|---|---|
| **MSIMULIZI** | Sasa ni miezi imepita. Malaika alipita mtihani wake bila ya kufanya udanganyifu. Na sasa amerejea kutoka masomo yake ya utendaji nyanjani ambako alipata fursa ya kutumia ujuzi aliousomea chuoni kuhusu masuala ya uhifadhi wa mazingira. Amereja chuoni mwa mwaka wake wa mwisho na mtihani uko karibu, kumaanisha ana muda wa wiki chache tu kabla ya kufanya mtihani wake wa mwisho. Pia Rafiki yake Cindy yaonekana amepata funzo.. |

SCENE 4: ***CHUMBANI KWA CINDY NA MALAIKA***

| | |
|---|---|
| MALAIKA | Cindy, kwa nini tusipange utaratibu wa kusoma pamoja? |
| CINDY | Hilo ni wazo zuri. Pia mimi nina wazo jingine. |
| MALAIKA | Hebu niambie. |
| CINDY | Mimi sidhani utaweza kusomea Mtihani wako wa mwisho ukiwa nyumbani huku kazi zote za kuchunga mbuzi na Ngombe zikikukodolea macho. |

MALAIKA Una maana gani. Hayo ndiyo maisha yangu. Ni lazima niwasaidie wazazi wangu na kazi za shambani.

CINDY Namaanisha hivi...

MALAIKA Kwa hivyo...?

CINDY Unaonaje ukiishi hapa jijini kwa muda wa wiki kadhaa hivi...

MALAIKA **(*akimkatiza)*** Hapana, hilo haliwezekani.

CINDY Hebu subiri, nisilikize! Unaweza kuja kuishi na sisi nyumbani kwetu.

MALAIKA (***akiwa amesisimkwa****)* Kweli, unaweza kunialika tafadhali?

CINDY Usiwe mpumbavu ! Tumeishi na wewe katika chumba kimoja kwa muda mrefu sana ama sivyo?

MALAIKA Lakini kwa sharti moja tu….

CINDY Bado sijamaliza. Ukiwa unaishi na sisi nyumbani kwetu tutaweza kusoma pamoja na kutumia huduma za maktaba ya chuo na yale ya jiji. Pia tutaweza kukutana na wanafunzi wenzetu na kusoma pamoja.

MALAIKA Usifanye dhihaka… Cindy, siamini haya unayoniambia. Yaani wewe sasa umeacha kabisa wizi wa mtihani?

CINDY Ahh ahhh… unakubaliana nami au la?

MALAIKA Cindy, wewe ni rafiki wa dhati, nimekubali wazo lako. Lakini kwa sharti moja tu. Kwamba pia wewe utalikubali wazo langu.

CINDY Nakusikiza ..!

MALAIKA Kwamba wiki ya mwisho ya likizo yetu tutaandamana hadi kwetu kuwasalimia wazazi wangu. Kisha nitakufunza jinsi ya kukamua ng'ombe!

CINDY Hapana… mimi siwezi!

MALAIKA **(*akicheka)*** Sawa basi. Tutakamua mbuzi badala ya ng'ombe.

CINDY (*pia akicheka)* Hapana! Hapana! Hapana! au tupange kukutana na Daniel hapa mjini badala ya kufikiria kukamua ng'ombe na mbuzi?

**Muziki**

## OUTRO

**MSIMULIZI** Na kufikia hapo ndio tumefika mwisho wa kipindi chetu cha leo. Je Malaika ataweza kumudu maisha ya familia ya Cindy jijini? Na je, Cindy naye atayaweza maisha ya kijijini? Marafiki hawa sasa, kila mmoja amekuwa mnasihi wa mwenzake. Na je itakuwaje wakati wa mtihani wao wa mwisho? Ungana nasi kwa makala yajayo. Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki na vingine, tembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe. Kumbuka pia unaweza kukutumia maoni yako kuhusiana na yote uliyoyasikia. Hadi wakati mwengine. Kwa heri.